

# Umoja wa Mataifa



[www.un.org](http://www.un.org)



Sisi watu wa Umoja wa Mataifa



*Sisi watu*



# **Yaliyomo**



**1**

**Umoja wa Mataifa (UM) ni nini?..... 4**

**2**

**Historia ya Umoja wa Mataifa..... 6**

**3**

**Mkusanyiko mkubwa zaidi wa UM..... 8**

Mkutano Mkuu

**4**

**Kwa ajili ya amani na usalama duniani: ..... 10**

Baraza la Usalama.

**5**

**Kwa mafanikio ya kila mmoja:..... 12**

Baraza la Kiuchumi na kijamii.

**6**

**Vyombo vingine muhimu vya UM na kazi zake: 14**

Baraza la Udhagini, Mahakama ya Kimataifa,  
na ofisi ya Shughuli za Kiutawala

**7**

**Simulizi mbalimbali kuhusu Umoja wa Mataifa 16**

**8**

**Malengo ya Maendeleo ya Milenia ni nini?..... 21**

**9**

**Umoja wa Mataifa Tanzania..... 22**

# UM ni nini?

1

Nasikia "UM"  
kila wakati  
lakini ni nini?



Inafanya  
nini?

Ni  
mahali pa  
namna  
gani?



Enyi vijana!  
Nitawaambia  
habari za UM:  
Umoja wa  
Mataifa!



Wewe  
ni  
nani?


Mimi ni  
mwangalizi wa  
UM na nitakuwa  
kiongozi wenu.



4

## • Kengele ya Amani

Katika uga wa jengo la Ofisi ya Shughuli za Kiutawala mijini New York, ipo Kengele ya Amani iliyotolewa na Japani kama mchango wake na pia kama ishara ya kutaka amani duniani. Imekuwa desturi kengele hiyo kupigwa na Katibu Mkuu kila tarehe 21 ya Septemba, siku ya Kimataifa ya Amani.



# Historia ya Umoja wa Mataifa



Mnamo mwaka 1941,  
katika Vita vya Pili vya Dunia...



2  
Watu  
wengi sana  
wamepoteza  
maisha yao  
katika vita hii.

Tuunde dunia  
isiyokuwa na  
vita.

Franklin D. Roosevelt  
Rais wa Marekani  
(1933 – 1945)

Bwana Winston Churchill  
Waziri Mkuu wa Uingereza  
(1940 – 1945)

Tujadili jambo hili  
na nchi nyingine.

Mwaka  
1945,  
viongozi  
wa nchi 50  
walikutana mjiini  
San Francisco,  
Marekani.

Tuanzisheni  
jumuia ya  
Kimataifa.






### • Nembo ya UM

Ramani ya dunia iliyozungushwa  
shada la matawi ya mizeituni,  
ishara ya amani.



Kwa hiyo, tarehe 24 Oktoba watu duniani kote wanaadhimisha siku ya Umoja wa Mataifa (siku ya UM).



# Mkusanyiko mkubwa zaidi wa UM:

## Mkutano Mkuu

UM unafanya  
nini? Inafanya  
kazi namna  
gani?



Kwanza kabisa,  
UM unavyo vyombo sita  
vinavyochukua  
maamuzi



Chombo muhimu  
zaidi ni Mkutano  
Mkuu, ambao nchi  
wanachama wote  
wanakutana



3



Unaone-  
kana  
namna  
hii.

Mkutano Mkuu  
unakutana  
kila mwaka  
kuzungumzia  
masuala mengi

8

## • Lugha Sita Rasmi za UM



Kichina	Paz 和平	Kiarabu السلام
Kihispania Paz	Kifaransa Peace	Kirusi صلح
		Kiingereza Peace



## Kwa ajili ya amani na usalama duniani:

### Baraza la Usalama



• Wanachama watano wa kudumu wa Baraza la Usalama

Nchi hizi tano zinayo haki ya kupiga kura ya "hapana", inayoitwa "kura ya turufu".



Baraza la Usalama linaweza kukutana muda wowote na lina wanachama 15 wanaoweza kupiga kura: wanachama watano wa kudumu na wanachama kumi wasio wa kudumu.



Wanachama wa kudumu ni nani?

Wanachama wa kudumu ni China, Ufaransa, Jumuiya ya Urusi, Uingereza na Marekani



Wanachama wasio wa kudumu wanacha-guliwa kila miaka miwili na Mkutano Mkuu

Katika wale wanachama 15, tisa wanapaswa kupiga kura kuitisha maamuzi. Lakini iwapo mwanachama wa kudumu mmoja tu atapiga kura ya turufu, maamuzi hayatapita Baraza la Usalama.



Oh! wanachama wa kudumu wana nguvu!

Ndiyo! Na wanachama wa UM wanapaswa kufuata maamuzi yaliyofikiwa na Baraza la Usalama

## Kwa ajili ya mafanikio ya kila mmoja:

### Baraza la Kiuchumi na Kijamii



## • Tuzo ya Amani ya Nobel

Mfumo wa UM na wawakilishi wamepokea Tuzo la Amani mara 13 kuanzia 1945-2005. Tuzo hili inapewa watu au jumuia zinazohimiza amani duniani kwa kusaidia nchi kuelewana vizuri zaidi



Ndiyo,  
UNICEF  
inamaanisha  
Mfuko wa  
Umoja wa  
Mataifa kwa  
Watoto na  
hutoa misaada  
kwa watoto  
katika nchi  
zinazoendelea



Vilevile kuna  
UNESCO, ambayo  
inamaanisha Jumuiya  
ya Umoja wa Mataifa  
inayoshughulikia  
Elimu, Sayansi  
na Utamaduni.  
UNESCO inalinda  
maeneo ya urithi ya  
dunia na kuendeleza  
elimu kwa ajili ya  
watoto kila mahali





Baraza la Kiuchumi na Kijamii  
linajumuisha tume tano za kimikoa  
kwa ajili ya Afrika, Asia na Pasifikasi,  
Ulaya, Amerika ya Kilatini na  
Karibiani, na Asia Magharibi



Sasa hivi,  
Baraza lina  
wanachama  
54 na  
linakutana  
mara moja  
kwa mwaka

# Vyombo vingine vya Umoja wa Mataifa na kazi zake

Baraza la Udhamini, Mahakama ya Kimataifa na Ofisi ya Shughuli za Kiutawala



## • Katibu Mkuu

### Mfululizo wa Makatibu Wakuu wa UM ni pamoja na:


1. Trygve Lie (Norway) 1946-1952
2. Dag Hammarskjold (Sweden) 1953-1961
3. U Thant (Myanmar) 1961-1971
4. Kurt Waldheim (Austria) 1972-1981
5. Javier Perez de Cuellar (Peru) 1982-1991
6. Boutros Boutros-Ghali (Egypt) 1992-1996
7. Kofi Annan (Ghana) 1997-2006




Chombo  
cha tano  
ni  
Maha-  
kama  
ya  
Kimataifa

UN

Nchi  
zinaweza  
kuleta  
malalamiko  
dhidi ya nchi  
nyingine  
mahakamani



Iko Hague,  
Uholanzi.  
Mahakama  
ina majaji  
15 ambaa  
wanateuliwa na  
Mkutano Mkuu  
na Baraza la  
Usalama



Chombo cha sita  
ni Sekretariati (Ofisi  
ya Shughuli za  
Kiutawala) ambayo  
ina karibu  
wafanyakazi 15,600  
(karibu 8,900 chini  
ya bajeti ya kawaida  
inayotolewa kutoka  
nchi 170). Mkuu wa  
Ofisi ya Shughuli za  
Kiutawala ni Katibu  
Mkuu ambaye  
anatawala mtandao  
wa UM

Katibu Mkuu anateuliwa na Mkutano Mkuu  
kwa mapendelezo ya Baraza la Usalama. Katibu  
Mkuu, kwa kawaida, hufanya kazi kwa kipindi  
cha miaka mitano kinachowezwa kurudiwa kwa  
vipindi viwili



# Simulizi Mbalimbali kuhusu Umoja wa Mataifa



United Nations Office  
for the Coordination of  
Humanitarian Affairs



UNITED NATIONS  
Office on Drugs and Crime



Sasa,  
twendeni  
tukaone baadhi  
ya shughuli za  
UM!

## Simulizi Mbalimbali kuhusu Umoja wa Mataifa

Pamoja nyakati za maafa.

Mamia ya maelfu ya watu wamepoteza maisha yao na mamilioni njia zao za kupata riziki zao kwa sababu ya majanga ya asili. UM ni muhimu katika kuratibu jithihada za kuleta faraja na kusaidia jamii kurudi katika hali ya kawaida baada ya maafa kama tsunami ya Bahari ya India, vimbunga, mafuriko, ukame, tetemeko za ardhi na tufani.



UM inatoa chakula, madawa, hifadhi na misaada kwa ajili ya kilimo, uvuvi, maji na miradi ya usafi kwa ajili ya kusaidia jamii kuanza kuishi tena maisha yao ya kawaida. Shirika la Afya Duniani linafuatilia afya ya umma ili milipuko ya magonjwa kama kupooza yaweze kudhibitiwa.

Mpango wa Chakula Duniani wa Umoja wa Mataifa (WFP) na Tanzania wanatumia msaada wa chakula kwa ajili ya kuokoa maisha na njia za kujipatia riziki za watu walioathirika na majanga na kwa ajili ya kutoa chakula kama uwekezaji katika sekta ya kilimo, elimu na afya.

### Sarah afurahia maji safi (Malawi, Africa)

Maisha ya Sarah Phiri yamebadilika kabisa tangu jamii yake iamue kuchimba kisima pekecho kipyä katika kijiji chao cha Mzikawola, Malawi, kabla ya kisima, alivyosema Sarah, "wanawake wa kijiji walipashwa kutembea kwa saa nzima kwenda na kurudi mtoni kwa ajili ya kupata maji safi".



Zaidi ya uchovu wa kimwili kwa kutembea mbali hivo, Sarah aliongeza kwamba hali ya maji ilikuwa mbaya sana." Tulisumbuliwa na magonjwa mengi. Sasa hivi hapana."

Masaa wawili ya ziada ambayo wanawake wa kijiji cha Sarah wanaokoa kila siku kwa kutotembea umbali mrefu kwa ajili ya kwenda kutafuta maji yamefungua nafasi mpya. Sarah alisema wengine wanalima chakula zaidi kinachoboresha malezi na mapato ya familia. Chakula cha ziada kinauzwa sokoni au kubadilishwa na aina nyingine ya mazao. "Kisima cha kawaida tu kimeleta kila kitu, kuanzia amani ya mawazo mpaka maisha mazuri zaidi".

Malawi, anakoishi Sarah, ni moja ya nchi 49 maskini zaidi ulimwenguni. Zaidi ya nusu ya watu milioni 650 wanaoishi katika nchi hizo wanaishi kwa chini ya dola moja kwa siku. UM inasaidia mipango kama kuchimba visima kwa kuwawezesha watu kama Sarah na jamii yake.

## Simulizi Mbalimbali kuhusu Umoja wa Mataifa

### Haki ya kupata elimu India

Ndoto ya Aarti ya kupata kazi ilikaribia kuwa kweli wakati kijana huyu wa miaka 16 aliposhiriki katika mradi unaofadhiliwa na UNICEF-India wa kuwapatia elimu watoto wa mitaani. Aarti alilazimishwa kuacha shule akiwa na umri wa miaka 10. Alipitisha muda wa siku zake kwa kutafuta vibarua vya kila aina katika mji wa Mumbai na kuishi mitaani na mama yake na ndugu zake. Sasa msichana huyu anajifunza kufanya kazi ya kuuza maua na anajifunza kusoma na kuandika.



Ndoto ya Aarti ya kuwa na kazi nzuri ili kumsaidia mama yake na nduguze yaweza kuwa kweli. Wakati bado anakumbana na matatizo mengi, ameshinda la kwanza kwa kdai haki yake ya kupata elimu.

Tamko la Ulimwengu la Haki ya Binadamu linasema kwamba kila mtu anayo haki ya kupata elimu. Tume ya UM na Mawakala wa UM kama UNICEF, UNESCO, UNDP na UNFPA vinafanya kazi na Serikali na washirika kwa ajili ya kusaidia watoto kupata elimu huru na ya lazima yenye sifa nzuri na kuondoa tofauti za kijinsia katika elimu ya msingi na ya upili.

### Haki ya kupata elimu (Bolivia, Amerika Kusini)

Wahindi wa Guarani wanaishi Bolivia, Argentina, Brazil na Paraguay. Kuna miaka michache, viongozi wa Waguarani wa Bolivia walipeleka barua UM. "Miaka mingi iliopita", ilisema barua, "wakati shule zilifika mkoani mwetu, walituambia kwamba elimu ndiyo ingekuwa njia bora ya kututoa kwenye ushamba wetu. Tulijenga shule na kile kidogo tulichokuwa nacho na tukaifanya Serikali ipeleke waalimu. Lakini tumesubiri na hatujaona matunda ya hizo shule".



Elimu katika hizo shule ilikuwa yote katika lugha ya Kihispania. Serikali ilifikiri Kihispania kilikuwa kimeendelea zaidi kuliko lugha ya Kihindi na kwamba Wahindi walipashwa kujifunza hicho. Kwa bahati mbaya, badala ya kuwasaidia kuendelea, elimu ilifanya kinyume. Waalimu wengi waliwaambia watoto wa Waguarani, ambao hawakuweza kujifunza lugha mpya, kwamba walikuwa wapumbavu na washamba. Matokeo yake, watoto walivunjika moyo.

Mwaka 1989, mashirika mawili ya UM, UNICEF na UNESCO waliingilia kati kubadili hali hiyo. Wawakilishi wao walikutana na Waguarani na wajumbe wa Serikali ya Bolivia. Kwa msaada wa jumia nyingine kadhaa za ndani na za nje, walianzisha mpango mpya wa shule kwa ajili ya kuwapa watoto wa Waguarani nafasi ya kujifunza lugha mbili, Kiguarani na Kihispania. Hatua hii ililetä mafanikio.

Waguarani sasa wana mategemeo zaidi. Kama mzazi alivyoandikia UM, "Watoto wetu sasa wanajifunza zaidi na vizuri. Hatimaye wanaweza kujieleza kwa uhuru bila kuadhibiwa kwa kusema lugha yao wenyewe".

## Simulizi Mbalimbali kuhusu Umoja wa Mataifa

### Marafiki katika shida ni marafiki wa kweli (Afghanistan)

Msichana mdogo alisema alikuwa hajawahi kumiliki kitu cha kuchezza katika maisha yake. Sasa alikuwa akiruka kamba kwa furaha kwa mara ya kwanza. Watoto wengine wakimbizi wa Afghani walifungua kwa shauku zawadi zao za bei nafuu za penseli, penseli za rangi na daftari. Wasichana walisuka nywele zao vizuri kwa wiki kadhaa.

Miaka michache iliyopita, UM na Chama cha Dunia cha Wasichana Viongozi walianzisha mpango wa "Kifurushi cha amani". Kama mwitikio, wasichana katika nchi 52 walikusanya zaidi ya vifurushi 260,000 kwa ajili ya watoto wakimbizi duniani kote. Wasichana viongozi katika Japani waliamua kukusanya zawadi kwa ajili ya watoto wa Afghani. Miaka michache iliyopita, wasichana wengi wa Japani walikusanya vifurushi 13,536. Baadae, sita kati yao walikwenda kambini kwa ndege na waligawa vifurushi kwa familia za wakimbizi.



Wakati wasichana walipokuwa wanagawa vifurushi vyao, watoto wakimbizi walikuwa kivutio kwa kila mmoja. Mwalimu mmoja, aliyeawaangalia watoto ambao kwa kawaada ni waoga wakianza kuimba, alisema kwamba thamani ya hivyo vifurushi haikuwezekana kukadirriwa. Vinaweza kuwa vyao bei ndogo, lakini zawadi zilikuwa vityu vyenye thamani zaidi kwa watoto hawa. (Imenakiliwa kutoka gazeti la wakimbizi, linalochapishwa na shirika la wakimbizi la Umoja wa Mataifa).

### SUK Ratha apata matumaini (Cambodia)

Cambodia ni moja ya nchi zilizotapakaliwa na mabomu ya kutega zaidi duniani. Miongo mitatu ya vita na mapigano ya kiraimeacha mamilioni ya mabomu yaliyosambaa ndani ya nchi hii iliyofanywa kuwa maskini. Tangu 1979, zaidi ya Wakambodia 57,000 wameteseka kwa kukatwa viungo, wengi wao wakiwa watoto wasio na hatia. Mmoja wao ni Suk Ratha wenye umri wa miaka 15.



Mguu wa Suk Ratha ulikatwa baada ya msichana huyu kukanyaga bomu la kutega ardhini wakati akienda kwenye soko la eneo hilo. Hakujuu ataendeleaje, hata jinsi gani angefika nyumbani kwao, nyumba ndogo iliyokuwa imejengwa juu ya mironjo. Lakini jumuia au vyama vya watu binafsi vinavyosaidia waathirika wa mabomu ya kutega ardhini wamehakikisha anapata kiungo bandia, na atajifunza kutembea tena. Wamesaidia familia yake pia kwa kuipa vifaa vya shule kusaida Suk Ratha kubaki shulenii, na ng'ombe kwa ajili ya maziwa na mapato ya ziada.

Mashirika ya Umoja wa Mataifa yanafanya kazi pamoja kuondoa mabomu ya kutega ardhini, kuelimisha watu na kusaidia waathirika. Huduma ya vitendo kuhusu mabomu ya ardhini inasaidia jitihada za kuendeleza na kutekeleza makuballiano ya kukataza mabomu ya ardhini, ambayo yameidhinishwa rasmi na nchi 136 na yamesainiwa na nchi 148. Inarabibu pia kazi ya mashirika ya UM kama UNICEF na UNDP, kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali, pamoja na Msalaba Mwekundu wa Kimataifa, Kundi la kushauri kuhusu mabomu ya Ardhini na taasisi za serikali kama kituo cha Cambodia cha vitendo kuhusu Mabomu ya kutega Ardhini.

# Simulizi Mbalimbali kuhusu Umoja wa Mataifa

## Kulinda watoto (Viet Nam)



Thuy anaishi mitaani na kaka yake na mama yake nchini Vietram. Wanauzu makopo na chupa ili wapate pesa kwa ajili ya mama yao, ambaye ni mgonjwa. Thuy ameathirika na kutumikishwa oyo.

Hofu kubwa ya wasichana na wawulana wanaofanya kazi sana katika migodi yenye hatari, wakiwa wanauzwa na kufanyiwa biashara ya ukahaba, wakilazimishwa kufanya kazi masaa mrefu kama watumihi wa nyumbani, mashambani na karakana, imepeleka suala la kutumikisha watoto mbele ya macho ya Serikali na jamii ya kiraia.

UM inasaidia watoto kuondoka mitaani na inasimamia vibanda vya oyo ovyo kuhakikisha huduma za msingi zinapatikana, inaendesha mipango inayotoa malazi, elimu, mafundisho na uunganishaji wa familia. UNESCAP ni sehemu ya Mradi wa Ushirikiano wa UM kuhusu Biashara ya Wanawake na Watoto katika Wilaya ya Mekong, ambao unalenga nchi tano za Kusini Mashariki mwa Asia na Uchina.

Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO) na Mpango wake wa Kimataifa juu ya kuondosha kazi kwa Watoto limeanzisha kampeni duniani kwa ajili ya kuziomba Serikali kuthibitisha rasmi makubaliano juu ya aina mbaya zaidi za kazi za watoto. Kuna vilevile mikataba mingi ya UM na makubaliano juu ya Haki za watoto kwa ajili ya kulinda watoto na kuwaepusha na madhara. UM umetambua umuhimu wa watoto na umetangaza Mwongo wa Kimataifa kwa ajili ya Utamaduni wa Amani na kutokutumia nguvu kwa Watoto Duniani (2000 – 2010).



## Paul aokoa maisha (kutoka Mexico)

Kama vinyozi wengi duniani kote, Paul Lopez amejenga uhusiano wa karibu na wateja wake. Wanasiliza ushauri wake kuhusu mwonekano na wanajadiliana masuala binafisi. Lakini katika saluni yake huko Jiji la Mexico, Paul anafanya zaidi kuliko kubadilishana umbeya na kutoa madokezo ya urembo. Anatoa vilevile habari zinazoweza kuokoa maisha.

Paul amefunzwa chini ya Kampeni bunifu inayofadhiliwa na Umoja wa Mataifa huko Mexico kwa kuendeleza utambuzi mionganoni mwa wateja wake kuhusu VVU/UKIMWI. Kwa sababu wateja wao wanawasiliza, idadi kubwa zaidi na zaidi ya watengenezaji wa nywele na vinyozi ni washiriki muhimu katika Kampeni ya kuelimisha watu kuhusu ugonjwa huu na namna ya kujilinda wenyewe.

Kampeni, ambayo inaitwa "Kiungo cha Utepe Mwekundu na Uhai: Kuzuia VVU/UKIMWI", inasaidiwa na shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa na Mpango wa kudhibiti Ukimwi wa Umoja wa Mataifa. Umoja wa Mataifa inaendesha vikao maalum kwa ajili ya kujadili njia za kuzuia na kusimamisha kuenea kwa VVU/UKIMWI.



# Malengo ya Milenia ni nini?



Kufikia mwaka 2015, Nchi Wanachama wote 191 wa Umoja wa Mataifa wameahidi kufikia malengo haya.

## Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya UM

**Chunga ahadi  
Malengo ya  
Maendeleo ya  
Milenia.**



Mwezi wa Septemba 2000, Nchi zote wanachama zote zilipitisha kwa kauli moja Tamko la Milenia la Umoja wa Mataifa. Katika Tamko hilo, Serikali zilikubaliana kwamba zitajitahidi kwa uwezo wake kuwaondoa ndugu zao wanaume, wanawake na watoto kutoka hali ya umaskini mkubwa.




### Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MMM)


- 01 Kutokomeza umasikini uliokithiri na njaa
- 02 Elimu ya Msingi kwa wote
- 03 Usawa wa Kijinsia na fursa sawa kwa wanawake
- 04 Kupunguza vifo vyta watoto wachanga
- 05 Upatikanaji wa huduma bora za uzazi
- 06 Kupambana na Ukimwi, malaria na magonjwa mengine.
- 07 Kulinda mazingira yetu
- 08 Kujenga mshikamano wa kimaendeleo duniani.

[www.un.org/millenniumgoals](http://www.un.org/millenniumgoals)

# Umoja wa Mataifa nchini Tanzania



## Umoja wa Mataifa nchini Tanzania



# **Umoja wa Mataifa Tanzania**

## **UNDP**

Mpango wa Maendeleo  
wa Umoja wa Mataifa.

## **UNV**

Shirika la Kujitolea la Umoja  
wa Mataifa

## **UNHCR**

Shirika la Wakimbizi la  
Umoja wa Mataifa

## **FAO**

Shirika la Chakula na Kilimo  
Duniani

## **ILO**

Shirika la kazi la kimataifa

## **UNAIDS**

Mpango wa Pamoja wa  
Umoja wa Mataifa juu ya  
VVU/ UKIMWI

## **UNESCO**

Shirika la Elimu, Sayansi na  
Utamaduni la Umoja wa  
Mataifa

## **UNFPA**

Mfuko wa Watu wa  
Umoja wa Mataifa

## **UNIC**

Kitengo cha Habari  
cha Umoja wa Mataifa

## **UNICEF**

Shirika la Watoto  
la Umoja wa Mataifa

## **UNIDO**

Shirika la Maendeleo ya  
Viwanda la Umoja wa Mataifa

## **WFP**

Mpango wa Chakula Duniani

## **WHO**

Shirika la Afya Duniani

## **UNCDF**

Mfuko wa Maendeleo wa  
Umoja wa Mataifa

## **UN Habitat**

Mpango wa Makazi ya Watu  
wa Umoja wa Mataifa

## **UNICTR**

Mahakama ya Kimataifa ya  
Rwanda

## **IMF**

Shirika la Fedha Duniani

## **WB**

Benki ya Dunia



Kitengo cha Habari cha Umoja wa Mataifa  
Dar es Salaam, Tanzania

S.L.P. 9224, Eneo la Makazi ya Ghuba ya Msimbazi,  
Barabara ya Kingsway / Mafinga, Kitalu Na. 134-140,  
Kinondoni, Dar es Salaam.  
Barua pepe: unic.urt@raha.com  
Tovuti: [www.untanzania.org](http://www.untanzania.org)  
[www.unic.undp.org](http://www.unic.undp.org)